



NAETISL

National Association of
Educational Translators and
Interpreters of Spoken Languages



MODDC

Missouri
Developmental
Disabilities Council

Kuelewa Huduma Zinazohusiana: *Mwongozo wa Mzazi*

Funding for the Supporting Language Access in Schools Project in Missouri provided by the Missouri Developmental Disabilities Council, was supported by the Administration for Community Living (ACL), U.S. Department of Health and Human Services (HHS) as part of a financial assistance award totaling \$1,361,246 with 100 percent funding by ACL/HHS. The contents are those of the author(s) and do not necessarily represent the official views of, nor an endorsement, by ACL/HHS, or the U.S. Government.



naetisl@gmail.com

NAETISL



Follow us



MODDC



moddc@moddcouncil.org



www.naetisl.org

www.moddcouncil.org





Kuelewa Huduma Zinazohusiana: Mwongozo wa Mzazi

Huduma Zinazohusiana ni nini?

Huduma zinazohusiana ni huduma za usaidizi zinazotolewa ili kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu kufaidika na elimu maalum. Huduma mahususi zinajumuishwa kwenye Mpango wa Elimu ya Mtu Binafsi wa mwanafunzi (IEP) ikiwa timu itaamua kuwa mwanafunzi anazihitaji.

Ni mifano gani ya huduma zinazohusiana?

Huduma za kawaida zinazohusiana zinajumuisha:

- Tiba ya lugha ya kuongea
- Tiba ya kufanya kazi
- Tiba ya mwili
- Usafiri
- Ushauri na huduma za Kisaikolojia
- Huduma za ukalimani
- Huduma za teknolojia na usaidizi
- Huduma za kimatibabu (kwa madhumuni ya uchunguzi au tathmini)

Huduma za Usemi na Lugha

- Tiba ya lugha ya hotuba husaidia wanafunzi na:
- Utamkaji (jinsi sauti zinavyotoka)
- Ukuzaji wa lugha (kuelewa na kutumia lugha)
- Masuala ya sauti au ufasaha (kama kigugumizi)
- Ujuzi wa mawasiliano ya kijamii





Tiba ya Kazi (OT)

Tiba ya Kazi huwasaidia wanafunzi katika:

- Ujuzi wa kutumia vidole vya mkono (k.m., kuandika, kukata)
- Usindikaji wa hisia
- Ujuzi wa maisha ya kila siku (k.m., kuvaa nguo, kutumia vyombo)
- Uhuru katika mazingira ya shule

Tiba ya Mwili (PT)

Tiba ya mwili inalenga:

- Ujuzi wa kutumia misuli mikubwa ya mwili (k.m., kutembea, kupanda ngazi)
- Uwezo wa Kutembea na usawa
- Matumizi ya vifaa vya usaidizi (k.m., vitembezi au viti vya magurudumu)
- Ushiriki salama katika shughuli za shule

Huduma za Usafiri

Huduma hizi huakikisha kuwa mtoto anaweza kusafiri kuelekea na kutoka shuleni au kwenye program inayohusiana.

Hii inaweza kujumuisha:

- Basi maalum ama gari
- Msaidizi wa basi au mfuatiliaji
- Usafiri wa mlango hadi mlango
- Marekebisho kama vile lifti za viti vya magurudumu au viunga





Huduma za Ushauri au Kisaikolojia

Hizi zinajumuisha:

- Ushauri wa shuleni ama kazi ya kijamii
- Tiba ya kibinafsi ama kundi
- Mipango ya kuingilia tabia
- Uchunguzi wa kisaikolojia na msaada

Huduma za Ukalimani

Huduma hizi huwasaidia wananfunzi viziwi au wasiosikia vizuri ama wanaowasiliana katika lugha nyingine kando na Kiingereza kupitia:

- Wakalimani wa lugha ya ishara
- Wafasiri wa usemi wa Cued (Hotuba ya Cued ni aina ya lugha ya ishara) Wakalimani wa mdomo
- Ufikiaji wa Mawasiliano kwa Wakati Halisi (CART). (CART ni huduma inayotoa unukuzi wa papo hapo wa lugha inayozungumzwa hadi maandishi yaliyoandikwa)

Teknolojia ya usaidizi (AT)

Teknolojia ya usaidizi humsaidia mwanafunzi kupata mtaala na kuweza kuwasiliana. Mifano ni pamoja na:

- Vifaa vya mawasiliano
- Kibodi au program zinazojirekebisha
- Visaidizi vya kuona
- Vyombo ama vifaa maalum

Huduma za Kiafya na Matibabu

Huduma ambazo ni muhimu kiafya kwa mwanafunzi kuhudhuria shule na kujifunza, kama vile:





- Kupeana madawa
- Kufuatilia afya (k.m., kwa kisukari au mishtuko ya moyo)
- Uchunguzi unaofanywa na mtaalamu wa kimatibabu (kwa mpango wa IEP)

Nani huamua ni huduma gani inayohusiana ambayo mtoto wangu atapokea?

Timu ya IEP, inayojumuisha wazazi, hutathmini mahitaji ya mtoto na kuamua ni huduma gani inayohitajika kusaidia elimu yao. Hizi huduma zinaorodheshwa na kuelezwa kwenye IEP.

Ni nani anayetoa huduma hizi?

Usemi na lugha, OT, PT, na ushauri na huduma za kisaikolojia lazima zitolewe na wataalamu waliohitimu na walioidhinishwa.

Bado una maswali?

Onge ana meneja wa kesi wa mtoto wako, mwanasaikolojia wa shule, au timu ya IEP. Pia unaweza kuomba tathmini iwapo unafikiria mtoto wako anahitaji huduma inayohusiana.

Nawezaje kupata usaidizi kwa lugha yangu?

Omba huduma za mkalimani katika shule yam toto wako au katika ofisi za wilaya ya shule. Omba taarifa iliyotafsiriwa na kuandikwa iwapo utaihitaji. Taarifa inayopatikana kwa wazazi wote katika wilaya ya shule inafaa kupatikana kwako pia.

